JARIDA LA RS RUVUMA

TOLEO LA JULAI, 2026

RUVUMA YETU

Na. 0004

Tembelea ;www.ruvuma.go.tz

RUVUMA IVUME KWA MAENDELEO



RC RUVUMA AMPONGEZA BIRIATI YAFET KWA UFAULU WA JUU KIDATO CHA SITA

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, ameongoza hafla ya kumpongeza mwanafunzi Biriati Yafet mwenye mahitaji maalum na anayetokea katika mazingira magumu, baada ya kupata Daraja la Kwanza (Division I) kwa pointi 3 kwenye matokeo ya kidato cha sita mwaka 2026.

Katika hafla ya pongezi, Brigedia Jenerali Ahmed amesema tukio hilo liwe hamasa kwa wanafunzi wengine katika mkoa kusoma kwa bidii na kupata ufaulu wa juu. Amesema Biriati Yafet atatunukiwa zawadi ya shilingi milioni tatu na kusisitiza kuwa ataendelea kumfuatilia kwa ukaribu ili kuhakikisha anafikia malengo yake.

Katika hatua nyingine, amewataka viongozi wa elimu na jamii kuimarisha juhudi za kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum na wanaotokea katika mazingira magumu, akitolea mfano mchango wa Kalamu Education Foundation katika kumsaidia Biriati.

Kwa upande wake, Biriati Yafet, amesema mafanikio yake yametokana na nidhamu na bidii katika kusoma. Ameongeza kuwa ndoto yake kubwa ni kusoma nje ya nchi hivyo ameiomba serikali pamoja na mashirika mbalimbali kumsaidia kufanikisha malengo hayo, kwani anaamini atafanya vizuri sana.

Kwa upande mwingine, Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma, Dkt. Louis Chomboko, amesema mafanikio hayo yanapaswa kuwa chachu kwa wanafunzi wengine kuongeza bidi katika masomo.

Naye Kaimu Afisa Elimu Mkoa wa Ruvuma, Mwl. Mathias Tilia, amesema serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wanafunzi kama biriati ili waweze kupata elimu bora na kufikia malengo yao.

Kwa upande wake, Mratibu wa Kalamu Foundation, Said Bwanaally,



amesema lengo lao ni kuwapa matumaini wanafunzi wenye mahitaji maalum na wanaotokea katika mazingira magumu wajione wana uwezo wa kusoma na kufikia malengo yao.

Biriati Yafet Biriati ni mzaliwa wa wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma. Alisoma Shule ya Msingi Imani kata ya Lukumbule, kisha Songea Boys kwa kidato cha kwanza hadi cha nne, na Ndanda Boys kwa kidato cha tano na sita.



JENGO LA ABIRIA UWANJA WA NDEGE SONGEA LAZINDULIWA



Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, amezindua rasmi jengo jipya la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Songea. Mradi ambao umegharimu shilingi milioni 842 na umekamilika kwa asilimia 100, ukiwa na uwezo wa kuhudumia abiria 300 kwa wakati mmoja.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Prof. Mbarawa amesema serikali inaendelea kuboresha viwanja vya ndege nchini ili kuendana na ongezeko la mahitaji ya usafiri wa anga kote nchini.

Amesisitiza kuwa kiwanja hiko ni mali ya Watanzania wote, hivyo ni wajibu wa wananchi kukilinda na kuhakikisha miundombinu yake inalindwa dhidi ya vitendo vinavyoweza kuhatarisha usalama wa huduma.

Prof. Mbarawa ametoa wito kwa mashirika ya ndege kutumia kikamilifu fursa ya uwanja wa Songea, ili kuongeza safari za ndege mkoani Ruvuma.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, ameiomba serikali kupitia Waziri wa Uchukuzi kujenga jengo lingine la kisasa zaidi katika Uwanja huo.

Amesema hatua hiyo ni muhimu itakayosaidia kuendana na kasi ya ukuaji wa sekta ya usafiri wa anga na mahitaji ya wananchi wa mkoa huo.

Amesisitiza kuwa jengo lililozinduliwa litumike kwa muda pekee, huku serikali ikiendeleza maandalizi ya ujenzi wa jengo jipya la kudumu, litakaloongeza uwezo wa kiwanja na kuchochea maendeleo ya kiuchumi katika Ruvuma

KATIBU TAWALA RUVUMA AWATAKA WAJASIRIAMALI WAJIFUNZE KABLA YA KUUZA

Badala ya kuishia kuuza bidhaa, wajasiriamali wa Ruvuma wametakiwa kutumia Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) kujifunza mbinu mpya zitakazowaongezea ushindani na kufungua masoko mapya.

Akizungumza baada ya kutembelea Banda la Mkoa wa Ruvuma katika viwanja vya Sabasaba, Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Bi. Mary Makondo, alisema maonesho hayo ni zaidi ya jukwaa la biashara; ni darasa la ubunifu, teknolojia na uongezaji thamani kwa bidhaa na huduma.

Ili kuonyesha umuhimu wa kujifunza kwa vitendo, Bi. Makondo aliambatana na wajasiriamali wa Ruvuma kutembelea banda la watengenezaji wa batiki kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ambapo walijifunza mbinu za kisasa za ubunifu na utengenezaji zinazoweza kuongeza ushindani wa bidhaa zao sokoni.

Alisisitiza kuwa mafanikio ya biashara yanategemea uwezo wa kujifunza, kujenga mitandao ya kibiashara, kutumia teknolojia na kuiga mbinu bora kutoka kwa wengine. Maonesho ya Sabasaba yanaendelea kuwa jukwaa muhimu linalowakutanisha wafanyabiashara, wawekezaji na wajasiriamali kutoka ndani na nje ya Tanzania, na hivyo kuharakisha ukuaji wa biashara na maendeleo ya uchumi wa Mkoa wa Ruvuma







RUVUMA IPO TAYARI KUKABILIANA NA EBOLA

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, amesema mkoa umeendelea kuimarisha maandalizi ya kukabiliana na ugonjwa wa Ebola kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, TAMISEMI na wataalamu wa sekta ya afya.

Akizungumza na Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Florence Samizi, ofisini kwake mjini Songea, RC Ahmed amesema tayari mkoa umetenga maeneo maalumu (Isolation Centers) kwa ajili ya wagonjwa watakaobainika, ili kulinda usalama wa wananchi wengine.

Amebainisha kuwa mkoa wa Ruvuma unapakana na nchi jirani na una uwanja wa ndege, hivyo hatua za tahadhari zimepewa kipaumbele ili kudhibiti uwezekano wa kuingia wagonjwa kutoka nje ya nchi.

Kwa upande wake, Dkt. Samizi amesema ingawa ugonjwa haujafika nchini, tahadhari ni jambo la msingi. Akisisitiza umuhimu wa Isolation Centers kuwepo karibu na mipaka ili wagonjwa wasisafiri umbali mrefu na kusababisha maambukizi mapya.

Ameeleza kuwa ufuatiliaji wa wagonjwa ni lazima uwe imara akitahadharisha kuwa bila ufuatiliaji sahihi, madhara yanaweza kuwa makubwa kwa jamii. Amesema watumishi wa afya walioko mstari wa mbele wanapaswa kupewa mafunzo ya kina, kwani wao ndio wako kwenye hatari kubwa ya kuathirika.

Vilevile, amehimiza ushirikishwaji wa jamii kupitia wahudumu wa afya ngazi ya jamii ili waweze kutambua dalili za Ebola na kutoa taarifa mapema kwa mamlaka husika akisisitiza ushirikiano wa wananchi ni nguzo muhimu katika kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo hatari

UJENZI WA BARABARA YA UTIRI–MAHANDE KUFUNGUA FURSA ZA KIUCHUMI

Ujenzi wa barabara ya Utiri–Mahande wilayani Mbinga yenye urefu wa kilometa 14.4, unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya kupitia programu ya AGRI-CONNECT, umeelezwa kuwa chachu ya kufungua fursa za kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma.

Mradi huo unaojengwa kwa kiwango cha lami na kutekelezwa na mkandarasi mzawa, Ovans Construction Company Limited, umefikia asilimia 83.5 ya utekelezaji, huku gharama yake ikiwa ni shilingi bilioni 16.5.

Akizungumza wakati wa ziara ya kukagua mradi huo, Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, amesema barabara hiyo inalenga kupunguza gharama za usafirishaji wa mazao ya kilimo, hususan kahawa, na kuimarisha mnyororo wa thamani wa mazao hayo katika soko la kimataifa.

Ameongeza kuwa serikali inaamini mradi huo utarahisisha usafirishaji wa mazao na kuwa kiungo muhimu cha kukuza uchumi wa kitaifa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, amesema barabara ya Utiri–Mahande itakuwa kichocheo cha uchumi na maendeleo ya wilaya ya Mbinga pamoja na vijiji jirani.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Mhe. Kisare Makori, amebainisha kuwa zaidi ya asilimia 85 ya wananchi wa wilaya hiyo wanajishughulisha na kilimo, huku kahawa ikiwa zao kuu linaloingiza mapato makubwa kwa kaya binafsi, vyama vya ushirika (AMCOS), na halmashauri kupitia ushuru wa mazao.

Ameeleza kuwa mradi wa barabara hiyo utarahisisha usafirishaji wa pembejeo mashambani na mazao baada ya mavuno kwenda masokoni, hivyo kuongeza tija kwa wakulima.

Kwa upande mwingine, Meneja wa TARURA Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Silvester Chinengo, amefafanua kuwa utekelezaji wa mradi ulianza Novemba 12, 2024 na awali ulikuwa umepangwa kukamilika Mei 29, 2026. Hata hivyo, kutokana na changamoto za mvua nyingi, muda wa utekelezaji umeongezwa na sasa mradi unatarajiwa kukamilika rasmi Agosti 20, 2026.





Muonekano wa Maporomoko ya Nakatuta katika mto Ruvuma ndani ya pori la Liparamba

BILIONI 9.2 ZABADILI MAISHA, SAFARI ZA HOFU ZABAKI HISTORIA

Miaka ya kusubiri imefikia mwisho. Wananchi wa Kijiji cha Mitomoni, Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, sasa watanufaika na usafiri salama mwaka mzima baada ya Serikali kuzindua Daraja la Mitomoni, mradi wa Sh bilioni 9.2 uliotekelezwa kwa ushirikiano na Benki ya Dunia.

Wakazi wanasema daraja hilo linafuta historia ya kuvuka mto kwa hatari, iliyokuwa ikisababisha vifo na kukwamisha usafirishaji wa mazao kila msimu wa mvua.

Sasa wanatarajia biashara kukua, gharama za usafiri kushuka na huduma za afya kufikika kwa haraka zaidi.

Akizindua mradi huo, Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, alisema daraja hilo litapunguza muda wa safari, kuimarisha huduma za afya na elimu, pamoja na kuunganisha kwa ufanisi Wilaya za Songea na Nyasa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, alisema mradi huo ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi wa mkoa. Naye Meneja wa TANROADS Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Saleh, alisema daraja lina urefu wa mita 45, limeunganishwa na barabara za kilomita 8.8, makaravati 14 na taa za barabarani, huku mkandarasi akilipwa asilimia 100 ya gharama za mradi.

Daraja hili linafungua fursa mpya za maendeleo na kuhakikisha Mitomoni inapitika kwa usalama katika misimu yote ya mwaka





BILIONI 80 KUBADILI BIASHARA KATI YA TANZANIA, MALAWI NA MSUMBIJI

Bandari ya Kimkakati ya Mbamba Bay mkoani Ruvuma utekelezaji wake umefikia asilimia 60 ya ujenzi, huku mradi wa zaidi ya Sh bilioni 80 ukitarajiwa kuibadilisha Ziwa Nyasa kuwa lango jipya la biashara na uwekezaji kati ya Tanzania, Malawi na Msumbiji.

Akizungumza baada ya kukagua maendeleo ya mradi huo Wilayani Nyasa, Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, alisema bandari hiyo itaongeza ufanisi wa usafirishaji wa mizigo, kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Mkoa wa Ruvuma na Taifa. Pia aliitaka Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kumsimamia mkandarasi kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati na kwa ubora unaostahili.

Kwa mujibu wa Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Erick Madinda, mradi unatarajiwa kukamilika Februari 2027, ukiwa na uwezo wa kuhudumia meli mbili za tani 5,000 kwa wakati mmoja na umejengwa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Wananchi wa Nyasa wameipongeza Serikali kwa uwekezaji huo, lakini wameomba ujenzi wa reli inayounganisha bandari uharakishwe ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo na kulinda barabara dhidi ya uharibifu unaoweza kusababishwa na magari mazito.



NKOSI MGENDELA GAMA AITANGAZA TANZANIA KUPITIA UTAMADUNI WA WANGONI

Utamaduni wa Wangoni umeendelea kung'ara kimataifa baada ya Inkosi Mgendela Gama wa Songea, Tanzania, kushiriki Tamasha la Sanjo ya Busiya (7-7 Fest), hatua inayotajwa kuimarisha juhudi za kuhifadhi urithi wa Kiafrika na kuunganisha jamii kupitia diplomasia ya utamaduni.

Katika tamasha hilo, Inkosi Mgendela Gama alikutana na viongozi wa jadi, wadau wa utamaduni na wawakilishi kutoka nchi mbalimbali za Afrika, wakibadilishana uzoefu kuhusu mbinu za kulinda na kurithisha tamaduni za asili.

Kupitia nyimbo na ngoma za Kingoni, aliutangaza utamaduni wa Wangoni mbele ya washiriki wa tamasha, akionesha nafasi ya sanaa katika kuhifadhi utambulisho wa jamii.

Kwa mujibu wa Ngoni Heritage Development Foundation, ushiriki huo umeongeza mtandao wa ushirikiano wa kitamaduni na kuhamasisha programu za kuwajengea vijana uelewa wa historia na mila za Wangoni.

UNESCO inaeleza kuwa urithi wa utamaduni usioshikika ni nyenzo muhimu ya kuimarisha mshikamano wa jamii na maendeleo endelevu.

Akizungumza baada ya tamasha, Inkosi Mgendela Gama alisema ataendelea kuimarisha elimu ya utamaduni wa Songea na kuwashirikisha vijana katika programu za kubadilishana tamaduni ili kulinda urithi huo kwa vizazi vijavyo.





HUDUMA YA KUSAFISHA DAMU YAANZA SONGEA: TUMAINI JIPYA KWA WAGONJWA WA FIGO RUVUMA

Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na maeneo ya jirani sasa hawatalazimika kusafiri mamia ya kilomita kutafuta huduma ya kusafisha damu (dialysis), baada ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea kuanza rasmi kutoa huduma hiyo kwa kutumia vifaa vya kisasa na wataalamu wenye uzoefu.

Uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea (HOMSO) umesema huduma hiyo inalenga kupunguza muda wa kusubiri matibabu, gharama za usafiri na kuongeza upatikanaji wa huduma muhimu kwa wagonjwa wa figo. Hospitali imewataka wananchi kufika mapema kwa uchunguzi ili kuongeza nafasi ya matibabu yenye mafanikio.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), magonjwa ya figo ni miongoni mwa magonjwa yasiyoambukiza yanayoendelea kuongezeka duniani, huku utambuzi wa mapema ukitajwa kuwa njia muhimu ya kupunguza madhara na vifo vinavyoweza kuzuilika.

Kuanzishwa kwa huduma hii kunatarajiwa kuimarisha huduma za kibingwa katika Mkoa wa Ruvuma na kuwapa wagonjwa fursa ya kupata matibabu karibu na makazi yao bila safari ndefu.





TAASISI KUBWA RUVUMA ZATUMIA NISHATI SAFI

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, amesema taasisi zote kubwa mkoani humo, ikiwemo shule na magereza, zimeacha kutumia kuni na mkaa na kuanza kutumia nishati safi kama gesi na majiko banifu ili kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Akizungumza na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dkt. Richard Stanslaus Muyungi, RC Ahmed ameeleza kuwa mkoa unaendelea na harakati za upandaji miti, ulinzi wa vyanzo vya maji hususan Mlima Matogoro, pamoja na ufuatiliaji wa biashara ya kaboni.

Amesema juhudi zinaendelea katika ukusanyaji wa taka ngumu kupitia vizimba maalumu, ingawa changamoto bado ipo kwenye uchakataji wake. Kupitia ushirikiano na NEMC, elimu ya utunzaji wa mazingira inaendelea kutolewa kwa wananchi na inapokelewa kwa mwitikio chanya katika kampeni za upandaji miti.

Kwa upande wake, Dkt. Muyungi amesema mazingira ni nguzo muhimu katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050, akisisitiza umuhimu wa nishati safi ya kupikia ili kufikia lengo la Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ifikapo mwaka 2034.

Pia ametaja fursa ya biashara ya kaboni kwenye misitu ya Ruvuma, ambapo makampuni yameanza kuonyesha nia ya kuwekeza.

Ziara ya Dkt. Muyungi mkoani Ruvuma inalenga kukagua hali ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kuimarisha ushirikiano na uongozi wa mkoa katika masuala ya nishati safi na biashara ya kaboni, pamoja na kutambulisha mikakati ya kitaifa ikiwemo kampeni ya Muungano Caravan na Mkakati wa Mageuzi ya Kijani





WABUNGE WA RUVUMA WATOA MSIMAMO HAKI, USALAMA NA UTU WA WAFANYAKAZI WA MRADI WA BARABARA VISIPUUZWE

Zaidi ya Sh bilioni 150 zinawekezwa katika ujenzi wa barabara ya lami nzito kutoka Songea hadi Lutukira yenye urefu wa km 100) na barabara ya mchepuko (km 16), mjini Songea huku Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma wakisisitiza kuwa mafanikio ya mradi huo hayawezi kupimwa kwa kasi ya ujenzi pekee, bali pia kwa namna haki, utu na usalama wa wafanyakazi vinavyolindwa.

Baada ya kukagua maendeleo ya mradi, wabunge hao walitaka mkandarasi na wadau wote kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya kazi ili kuongeza tija, ufanisi na kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati kwa manufaa ya wananchi.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Saleh Juma, alisema mradi umefikia asilimia 10, huku kazi za awali zikiendelea katika maeneo mbalimbali.

Alisisitiza kuwa TANROADS itaendelea kusimamia utekelezaji wake kwa karibu ili kuhakikisha unazingatia viwango vya ubora, muda na usalama.

Mradi huo unatarajiwa kuboresha usafiri, kuchochea biashara na kufungua fursa mpya za kiuchumi kwa maelfu ya wakazi wa Mkoa wa Ruvuma.





WANANCHI SONGEA WAOMBA ONGEZEKO LA BEI YA MAJI: "LILINDE MAISHA YA MWENYE KIPATO CHA CHINI

Pendekezo la kuongeza bei ya maji katika Manispaa ya Songea Mkoani Ruvuma limeibua mjadala huku wananchi wakitaka Serikali na mamlaka husika kuweka mbele ustawi wa kaya zenye kipato cha chini kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho.

Katika kikao cha kupokea maoni kuhusu ombi la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA), wananchi walionya kuwa ongezeko la bei kutoka Sh1,730 hadi Sh2,700 kwa kila mita ya ujazo ni sawa na ongezeko la takriban asilimia 56, hatua wanayohofia inaweza kuongeza idadi ya wateja wanaoshindwa kulipa bili na kuwalazimu kurejea kutumia maji ya visima visivyo salama.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, alisema ongezeko la watu, makazi na shughuli za kiuchumi limeongeza mahitaji ya maji, hivyo ni muhimu kuwepo uwiano kati ya uwezo wa wananchi kumudu gharama na uwekezaji wa kuboresha huduma.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Usambazaji Maji wa SOUWASA, Mhandisi Jafari Yahaya, alisema mapendekezo hayo yatalenga kufadhili ukarabati wa km 32 za mabomba chakavu, upanuzi wa mtandao kwa km 194, ujenzi wa vyanzo vipya, matenki, mitambo ya kutibu maji na ufungaji wa mita mpya.

Naye Meneja wa EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Walter Christopher, alisema mapitio ya bei hufanyika kwa mujibu wa utaratibu wa EWURA ili kuhakikisha huduma zinaendelea kuwa endelevu.

Uamuzi wa mwisho unatarajiwa kuzingatia maoni ya wananchi pamoja na hitaji la kuboresha huduma za maji bila kuwaongezea mzigo watumiaji.





MWENYEKITI TUNDURU AWASISITIZA WAZAZI KUWEKEZA KWA WATOTO

Mustakabali wa watoto ulitawala mjadala katika Kijiji cha Imani baada ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma Mhe. Seifu Dauda, kutoa wito kwa wazazi na walezi kuhakikisha kila mtoto anapata elimu na malezi bora, akisisitiza kuwa uwekezaji kwa mtoto leo ni msingi wa maendeleo ya jamii kesho.

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Lukumbule, Mhe. Dauda alisema watoto wanapaswa kuandikishwa na kuhudhuria shule kwa wakati, huku akiwataka wazazi kushirikiana kwa karibu na walimu kufuatilia maendeleo yao ya kitaaluma.

Wananchi walioshiriki mkutano huo walimpongeza Mhe. Dauda kwa kusikiliza kero zao na kuahidi kutekeleza maelekezo yaliyotolewa ili kuboresha elimu na malezi ya watoto katika kijiji hicho





Muonekano wa mnara wa makumbusho ya Taifa majimaji wa mashujaa 67



NAMTUMBO YAFUNGUA FURSA KWA VIJANA KUPITIA KILIMO CHA ALIZETI

Kilimo cha alizeti ni fursa ya ajira, biashara na kuongeza thamani kwa vijana wa Namtumbo mkoani Ruvuma.

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Mheshimiwa Ngollo Malenya, amepokea ujumbe kutoka Southern Sunflower Integrated Ecosystem, unaoongozwa na Dkt. Timothy Lyanga, akiambatana na Dkt. Mbiki Msumi, katika juhudi za kuhamasisha kilimo cha alizeti, kuwawezesha vijana na kuunganisha wakulima na masoko yenye tija.

Msisitizo wa mpango huo ni kujenga mnyororo wa thamani kuanzia uzalishaji wa mbegu, kilimo, uchakataji hadi upatikanaji wa masoko ili mkulima asibaki muuzaji wa malighafi pekee, bali awe sehemu ya uchumi unaoongeza thamani.

Tafiti za sekta ya kilimo zinaonesha kuwa kuongeza thamani na kuunganisha wakulima na masoko ni miongoni mwa njia muhimu za kuongeza kipato, ajira na ushindani wa mazao ya kilimo.



"BARABARA HII INANINYIMA USINGIZI!" — JUDITH KAPINGA AWEKA KIPAUMBELE CHA KWANZA MBINGA VIJIJINI

"Barabara ya Kitai–Ruanda inaninyima usingizi." Kauli hiyo ya Waziri wa Viwanda na Biashara na Mbunge wa Mbinga Vijijini, mkoani Ruvuma Mhe. Judith Kapinga, imeweka wazi ajenda yake kuu ya miundombinu: kukamilisha barabara hiyo kabla ya kuelekeza nguvu kwenye miradi mingine.

Akizungumza na wananchi wa Luhagara, Kata ya Litumbandyosi, Kapinga aliomba imani ya wananchi huku akiahidi kuendelea kuifuatilia kwa karibu. "Kipaumbele changu namba moja ni barabara hii," alisema.

Pamoja na miundombinu, alisisitiza uwajibikaji wa viongozi, akitaka taarifa za mapato na matumizi zisomwe hadharani kwa mujibu wa sheria. Pia alionya migogoro isiyo na tija, akisema inakwamisha maendeleo.

Kapinga aliiagiza Halmashauri kufanya tathmini ya ujenzi wa bweni la Sekondari Luhagara, huku akiwataka wazazi kuhakikisha watoto wanahudhuria shule na kutumia fursa za elimu.

Ziara hiyo, iliyohudhuriwa pia na TARURA, TANESCO, Mamlaka ya Maji na viongozi wa Halmashauri, ilihitimishwa kwa msaada wa jezi na vifaa vya michezo kwa vijana.

Kwa Mbinga Vijijini, ujumbe umebaki mmoja: maendeleo yanahitaji barabara, uwazi na uongozi unaowajibika.











SONGEA YAZALISHA TANI 90 ZA TAKA KILA SIKU—UCHAFU HUO SASA KUGEUKA FURSA YA AJIRA NA MBOLEA

Kila siku, Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma huzalisha takribani tani 90 za taka sawa na zaidi ya tani 2,700 kwa mwezi. Hata hivyo, uwezo wa sasa wa ukusanyaji ni takribani tani 75 kwa siku, pengo linaloacha takribani tani 15 zikisubiri ukusanyaji wa siku inayofuata.

Kwa Manispaa ya Songea taka si uchafu pekee. Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Udhibiti wa Taka na Usafi wa Mazingira manispaa ya Songea Amani Mmasi, anasema mpango mpya unalenga kuchakata taka zinazooza kuwa mbolea ya asili, huku plastiki na chupa zikielekezwa kwenye urejelezaji.

"Tunataka taka ziwe chanzo cha ajira na kipato," anasema Mmasi.

Hata hivyo Changamoto bado ipo. Katika Soko la Bombambili, mfanyabiashara Saidi Katoto anasema taka huongezeka zaidi wakati wa masika, huku Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, akisisitiza kuwa usafi lazima uende sambamba na mipango bora ya miji.

Kwa mujibu wa Mmasi, taka husafirishwa kutoka katikati ya mji hadi Dampo la Subira, lenye takribani hekari 98, huku mpango wa kuongeza magari manne ya ukusanyaji ukiwa katika hatua za mwisho.



MVUA HAZITAKIWI KUWA KISINGIZIO: TARURA YAMPA MKANDARASI WA DARAJA LA MUUNGANO AGIZO ZITO

Mvua zinazonyesha wakati wa masika zimekuwa zikichelewesha ujenzi wa Daraja la Muungano, wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma lakini Kamati ya Ukaguzi ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) imesema changamoto hiyo haiwezi kuwa sababu ya mradi kuchelewa kukamilika.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Henry Kaywanga, amemtaka mkandarasi kuongeza kasi, nguvu kazi na rasilimali ili kukamilisha daraja hilo kwa wakati uliopangwa.

Kwa mujibu wa Meneja wa TARURA Wilaya ya Namtumbo, Mhandisi Fabian Lugalaba, daraja hilo la zege lenye urefu wa mita 30 litakapokamilika litawaunganisha wakazi wa Minazini na Muungano, wakiwemo wanafunzi wa Shule ya Msingi Ukombozi, ambao hukumbwa na changamoto ya mafuriko na kukatika kwa mawasiliano wakati wa masika.

Mkazi wa Muungano Said Athumani amesema mradi huo utachochea shughuli za kiuchumi na kuboresha upatikanaji wa huduma za kijamii kwa kuwaunganisha wananchi mwaka mzima.

Ziara hiyo pia ilikagua ujenzi wa Daraja la Mtyangimbole–Mnadani. Sasa macho ya wananchi yako kwa mkandarasi: daraja likamilike kwa wakati.





WAKULIMA TUNDURU WAFUNGULIWA NJIA MPYA YA SOKO: AMCOS ZA WENJE NA MKALIMBE ZAPATA USAJILI KAMILI

Hatua ya usajili kamili wa AMCOS za Wenje na Mkalimbe imefungua ukurasa mpya kwa wakulima wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma baada ya vyama hivyo kukabidhiwa rasmi vyeti vya usajili .

Akizungumza katika hafla hiyo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Tunduru, Milongo Sanga, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya, amewataka wanachama kuimarisha vyama hivyo na kuwahamasisha wakulima wengine kujiunga ili wanufaike na mfumo rasmi wa ushirika.

Sanga amesema baada ya usajili, mazao yanapaswa kukusanywa na kuuzwa kupitia AMCOS kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa hatua inayolenga kuongeza kipato cha wakulima, kuimarisha uchumi wa maeneo hayo na kudhibiti utoroshaji wa mazao.

Amesisitiza pia umuhimu wa kuchagua viongozi waadilifu na wawajibikaji ili kulinda maslahi ya wanachama.



MABADILIKO MAKUBWA KWENYE KAHAWA MBINGA: HALMASHAURI YAANZA KUJIANDAA NA MICHE MILIONI 2.5

Kahawa si zao la biashara pekee kwa wakulima katika Halmashauri ya wilaya ya Mbinga Mkoani Ruvuma bali pia ni chanzo muhimu cha mapato ya Halmashauri na kiungo cha maendeleo ya wakulima.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Joseph Kashushura, wakati wa kikao na viongozi wa vyama vya ushirika (AMCOS) kuelekea ufunguzi wa msimu mpya wa mavuno ya kahawa.

Kashushura amesema Halmashauri imejipanga kuzalisha miche ya kahawa milioni 2.5 kwa ajili ya kugawiwa kwa wakulima msimu ujao, huku akizitaka AMCOS kuanzisha vitalu vya miche ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka.

Amesisitiza uadilifu katika usimamizi wa msimu wa kahawa, matumizi ya pembejeo zinazotolewa kwa ruzuku ya Serikali na kuboreshwa kwa miundombinu ya barabara ili kurahisisha usafirishaji wa mazao.



Afisa Ushirika, Nuhu Selenge, amewataka viongozi wa AMCOS kuripoti kampuni zitakazonunua kahawa kinyemela, huku Afisa Mapato, Frank Ngole, akisisitiza ulipaji wa mapato kwa wakati.





MRADI WA SHILINGI BILIONI 22.9 WAFIKIA 14.51% PEKEE,MKANDARASI AONYWA

Mradi wa ujenzi wa Masoko ya Manzese A & B pamoja na Kiwanda cha Kusindika Chakula katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma wenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 22 umefikia utekelezaji wa asilimia 14.51 pekee, licha ya muda wa awali wa kukamilika kumalizika. Hayo yamebainika Julai 23, 2026, wakati Kamati ya Fedha na Uongozi ya Manispaa ya Songea ilipokagua mradi huo. Mhandisi Mshauri wa Mradi, Eng. Bakari Tupa, alisema mkandarasi ameongezewa muda wa miezi sita kuanzia Julai 23, 2026 hadi Februari 6, 2027 kukamilisha kazi zilizobaki.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea, Wakili Bashir Muhoja, amesema hajaridhishwa na kasi ya utekelezaji, akisema kuchelewa kwa mradi kunazuia huduma na kuwaathiri wafanyabiashara wanaotarajia kunufaika na masoko hayo.
Kamati imemtaka M/S China National Aero-Technology International Engineering Corporation kuongeza nguvu kazi, vifaa na rasilimali. Mkandarasi amekiri mapungufu na kuahidi kuongeza kasi ya ujenzi.
Sasa macho yote yako kwenye Februari 6, 2027: je, muda huu wa ziada utageuka kuwa mwisho wa ucheleweshaji ?



SONGEA YAIOMBA NHC KUJENGA NYUMBA PERAMIHO:

Uongozi wa Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma umeliomba Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuanzisha mradi wa ujenzi wa nyumba katika eneo la Peramiho, ukilenga kuongeza upatikanaji wa makazi bora na yenye gharama nafuu kwa wananchi na watumishi wa umma.



Ombi hilo limetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mhe. Wilman Kapenjama Ndile, mbele ya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Kaspar Mmuya, wakati wa kufunga Kliniki ya Ardhi na kugawa hati miliki katika Viwanja vya Tamasha, Peramiho.
Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya, mradi huo unaweza kuwa kichocheo cha maendeleo ya Peramiho kwa kuboresha makazi, kuvutia uwekezaji na kukidhi mahitaji ya nyumba kwa watumishi na wananchi.
Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Mhe. George Ponela, ameunga mkono ombi hilo, akisema ujenzi wa nyumba za NHC unaweza kusaidia kupunguza changamoto ya makazi na kuchochea ukuaji wa Peramiho kuwa kitovu cha huduma na shughuli za kiuchumi.
Kliniki ya Ardhi iliyodumu kwa siku kadhaa ililenga kusogeza huduma karibu na wananchi, kutoa elimu ya umiliki salama wa ardhi na kuwawezesha kupata hati miliki zenye ulinzi wa kisheria.
Sasa ombi limewekwa mezani utekelezaji wake unaweza kuamua kama Peramiho itabaki kuwa eneo la makazi au itageuka kuwa kitovu kipya cha maendeleo ya Songea.

ASILIMIA 90 YA WAGONJWA WA HIMOFILIA TANZANIA HAWAJAGUNDULIKA,SONGEA YAANZA MSUKUMO WA KUWABUA

Wakati maelfu ya Watanzania wanaweza kuwa wanaishi na Himofilia bila kujua, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea imeanzisha kliniki maalumu kwa lengo la kuwabaini wagonjwa mapema na kuzuia madhara makubwa ya ugonjwa huo.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa Kliniki ya Himofilia, Julai 21, 2026, Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dkt. Magafu Majura, amewataka wataalamu wa afya, walimu na jamii kushirikiana kuwaibua wenye dalili za ugonjwa huo na kuwafikisha hospitalini.



"Tutatumia nafasi ya ziada kutembelea taasisi nyingine, hasa shule, kufanya uchunguzi wa awali ili kuwabaini wenye viashiria mapema," amesema Dkt. Majura.

Kwa mujibu wa Katibu wa Chama cha Himofilia Tanzania, Abdallah Makalla, duniani mtu mmoja kati ya kila watu 10,000 anakadiriwa kuwa na Himofilia.

Hata hivyo amesema Tanzania inakadiriwa kuwa na wagonjwa takribani 6,700, lakini ni wagonjwa 677 pekee waliogundulika huku zaidi ya asilimia 90 wakikadiriwa kutotambuliwa.

Himofilia ni ugonjwa wa kurithi wa kuvuja damu unaosababishwa na upungufu wa vigandisha damu mwilini (clotting factors) kumtambua mgonjwa mapema kunaweza kuzuia kutokwa damu kupita kiasi, ulemavu wa viungo na madhara ya muda mrefu.



RUVUMA YAVUKA LENGO LA MAPATO, SASA YALENGA BILIONI 66.63

Mkoa wa Ruvuma umevunja rekodi ya ukusanyaji wa mapato baada ya kukusanya Sh bilioni 61 kati ya lengo la Sh bilioni 54 katika mwaka wa fedha 2025/2026 mafanikio yaliyosababisha mkoa huo kupewa lengo jipya la Sh bilioni 66.63 kwa mwaka 2026/2027.

Kwa kiwango cha taifa, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeongezewa lengo kutoka Sh trilioni 37 hadi Sh trilioni 41.8.

Meneja wa TRA Mkoa wa Ruvuma, Sylver Rutagwelera, amesema mkoa umeweka mikakati ya kuwafikia wafanyabiashara, kutoa elimu ya kodi na kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari na kwa wakati.

"Wananchi wanapaswa kujivunia kulipa kodi kwa wakati, kwa kuwa kodi ndiyo msingi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma za kijamii," amesema Rutagwelera.

Kutoka Sh bilioni 54 hadi Sh bilioni 61, Ruvuma imeonesha kuwa nidhamu ya ulipaji kodi inaweza kubadili uwezo wa mkoa kuchangia maendeleo. Sasa mtihani ni kufikisha Sh bilioni 66.63.

ZAIDI YA SHILINGI MILIONI 350 ZAGEUKA HUDUMA ZA AFYA, ELIMU NA MAJI MBINGA,LUHAGARA YAPATA ZAHANATI MPYA

Kwa wajawazito wa Luhagara, safari ndefu ya kutafuta huduma za afya za kisasa sasa ni historia.
Wananchi wa Kijiji cha Luhagara, Kata ya Lutumbandyosi, Mbinga, Ruvuma, wameanza kunufaika na zahanati mpya iliyojengwa na Jitegemee Holdings Company Limited kupitia mpango wa uwajibikaji kwa jamii (CSR), baada ya kwa muda mrefu kukabiliwa na changamoto ya kusafiri umbali mrefu kupata huduma za msingi.
Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi na Ujenzi ya kijiji, Marco Njerekera, alisema mradi huo umepunguza adha kwa wananchi, hasa wajawazito.



Mtumishi wa afya katika zahanati hiyo , Avelina Ngapunda, alisema jengo la zamani lilikuwa na mazingira hatarishi, ikiwamo kuingia mara kwa mara kwa nyoka; changamoto iliyopungua baada ya kuanza kutumika kwa jengo jipya.
Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Deogratias Laballa, alisema Jitegemee imetekeleza miradi ya CSR yenye thamani ya zaidi ya Sh milioni 350, ikiwamo zahanati, madarasa, mabweni, nyumba za walimu na miradi ya maji.
Waziri wa Viwanda na Biashara, Judith Kapinga, alisema ushirikiano wa Serikali na sekta binafsi ni muhimu katika kuharakisha maendeleo, huku kampuni hiyo ikiwa imechangia zaidi ya Sh bilioni 1 kupitia Service Levy katika Halmashauri ya Mbinga.
Kwa Luhagara, uwekezaji wa madini sasa unaonekana pia katika kituo kinachookoa muda, gharama na maisha.



SERIKALI YALENGA KUPIMA ARDHI NCHI NZIMA KUONDOA MIGOGORO

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Kaspar Mmuya amesema lengo kubwa la serikali kwa sasa ni kupima nchi nzima, kupanga matumizi ya ardhi na kuwamilikisha wananchi, taasisi binafsi na za serikali maeneo yao.
Akizungumza na Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mhe. Kapenjama Ndile, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Brig. Gen. Ahmed Abbas Ahmed, katika ofisi ya mkuu wa mkoa mjini Songea, Mhe. Mmuya amesema hatua hiyo itasaidia kila mmoja kutambua umiliki na matumizi ya eneo lake, hivyo kupunguza na kuondoa migogoro ya ardhi.
Amesema wizara kwa kushirikiana na serikali za mikoa na wilaya inashughulikia migogoro ya ardhi, huku akisisitiza kuwa ni haki ya wananchi kueleza kero na kukata rufaa kuanzia ngazi za chini hadi kwa mawaziri au Rais pale ambapo hawajaridhika na maamuzi.
Mmuya amebainisha kuwa migogoro mingi inasababishwa na mifumo dhaifu ya matumizi na usimamizi wa ardhi, ikiwemo migogoro ya mipaka, matumizi yasiyo sahihi ya ardhi na uzembe wa kutolinda maeneo kwa muda mrefu.
Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mhe. Kapenjama Ndile, amesema mkoa wa Ruvuma unajivunia utendaji wa mamlaka zake katika kushughulikia migogoro ya ardhi na kuimarisha usimamizi wa rasilimali hiyo muhimu. Amesisitiza kuwa mamlaka hizo zimekuwa zikifanya kazi kubwa na yenye matokeo chanya katika kutatua changamoto za ardhi.



RC RUVUMA AZINDUA OFISI MPYA YA UHAMIAJI MKENDA

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, leo Julai 28, 2026, amezindua ofisi mpya ya uhamiaji pamoja na nyumba ya Afisa Uhamiaji Mfawidhi katika kituo cha Mkenda - Nakawale mpakani mwa Tanzania na Msumbiji.

Akizungumza katika hafla hiyo, RC Ahmed amesema ofisi hiyo iliyogharimu zaidi ya shilingi milioni 240.8 kwa ufadhili wa serikali kuu na nyumba ya mtumishi iliyogharimu zaidi ya milioni 133.7 kwa ufadhili wa Shirika la Uhamaji Duniani (IOM), ni sehemu ya kuimarisha usimamizi wa mipaka ndani ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Amesema uwekezaji huo utasaidia kudhibiti changamoto za uhamiaji usio rasmi, biashara haramu, usafirishaji wa binadamu na bidhaa, pamoja na vitisho vya ugaidi na uhalifu wa kuvuka mipaka.

RC Ahmed amesisitiza kuwa jitihada hizi zinaendana na maono ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuimarisha usalama wa mipaka, kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi na kuongeza tija ya huduma kwa wananchi.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Dkt. Franklin Rwezemula, amesema serikali inaendelea kutoa fedha kwa ajili ya miradi ya vyombo vya ulinzi na usalama, ikiwemo Idara ya Uhamiaji ili kuboresha utendaji kazi wa vyombo hivyo.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Wakili Mary Gasper Makondo, amesema uwekezaji huo unasaidia diplomasia ya uchumi na kuimarisha ushirikiano wa kitaifa na kikanda.

Kwa upande mwingine, Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mhe. Kapenjama Ndile, amesema uwekezaji huo unalenga kuimarisha mahusiano ya kikanda na kuongeza ustawi wa biashara mpakani.

Nao wananchi wa eneo hilo, akiwemo Grace Ali, wameiomba serikali kujenga barabara ya lami ya Likuyufusi - Mkenda ili kuongeza mchango wa kiuchumi na kijamii na kuimarisha zaidi uhusiano wa Tanzania na Msumbiji.



JE, TANZANIA ITAFIKIA ASILIMIA 80 YA MATUMIZI YA NISHATI SAFI MWAKA 2034?

Matumizi ya mkaa mbadala sasa imekuwa mjadala unaogusa afya, uchumi na mustakabali wa Tanzania. Wakati Serikali ikilenga kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia kutoka asilimia 28.6 hadi 80 ifikapo mwaka 2034, Kampuni ya Jitegemee ya Mbinga mkoani Ruvuma imezalisha tani 951 za mkaa mbadala unaotokana na makaa ya mawe, huku tani 439 tayari zikisambazwa katika mikoa tisa ikiwemo Zanzibar.

Bosco Mabena, Mkurugenzi wa Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Makaa ya Mawe ya Jitegemee, anasema bidhaa hiyo imeidhinishwa na Shirika la viwango Tanzania TBS.

Naye Nolasco Mlay, Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia, anasisitiza elimu kwa wananchi ni msingi wa mafanikio ya mkakati huo.

Kwa mujibu wa IEA, watu bilioni 2 duniani bado wanatumia nishati chafu ya kupikia, huku takribani vifo milioni 3 vya mapema vikihusishwa na tatizo hilo kila mwaka.

Swali kubwa sasa si uwepo wa mbadala wa mkaa pekee, bali kama mkaa mbadala huo una ubora, usalama, gharama nafuu na uthibitisho wa kisayansi utakaomfanya kila Mtanzania kuuchagua kwa ujasiri





MASISTA KUTOKA ULAYA WATEMBELEA MAKAO MAKUU YA WANGONI, WAIMARISHA URAFIKI WA ZAIDI YA KARNE

Ziara ya Masista Wamisionari kutoka Ulaya katika Makao Makuu ya Wangoni, Maposeni wilayani Songea mkoani Ruvuma imeibua upya historia ya zaidi ya miaka 120 ya ushirikiano kati ya Kanisa Katoliki na Taifa la Wangoni.

Tarehe 19 Julai, Inkosi Yamakhosi Zulu Gama na Inkosi Mputa Gama waliwapokea wageni hao kwa heshima kubwa, wakishuhudia urithi wa utamaduni wa Wangoni kupitia ngoma za asili, maonesho ya mila, vyakula vya jadi na ukarimu unaolitambulisha Taifa la Wangoni.

Uhusiano huo ulianza mwaka 1898 baada ya kuanzishwa kwa Misheni ya Peramiho, ambayo imechangia kwa zaidi ya karne moja maendeleo ya elimu, huduma za afya, imani na ustawi wa jamii katika Mkoa wa Ruvuma. Licha ya athari za Vita vya Majimaji, ushirikiano kati ya Kanisa Katoliki na Wangoni umeendelea kukua kwa msingi wa maridhiano, heshima na huduma kwa jamii.

Ziara hiyo imekuwa alama ya kuendeleza urithi wa historia, kuimarisha mshikamano wa tamaduni na kuthibitisha kuwa urafiki wa kweli unaweza kudumu kwa vizazi





TAKUKURU KUCHUNGUZA TUHUMA DHIDI YA MWENYEKITI WA KIJIJI

Hatima ya tuhuma zinazomkabili Mwenyekiti wa Kijiji cha Kazamoyo wilayani Tunduru mkoani Ruvuma sasa ipo mikononi mwa TAKUKURU baada ya Katibu Tawala wa Wilaya hiyo , Ndugu Milongo Sanga, akimwakilisha Mkuu wa Wilaya, kuagiza uchunguzi wa kina kufuatia malalamiko yaliyowasilishwa na wananchi.

Katika mkutano wa hadhara uliohudhuriwa na Kamati ya Usalama ya Wilaya, wananchi walieleza hoja zao kuhusu madai ya matumizi mabaya ya ofisi ya umma.

Sanga alisema uamuzi wa wananchi wa Julai 27, 2026 wa kumsimamisha Mwenyekiti haukufuata taratibu za kisheria, hivyo uchunguzi wa TAKUKURU utasaidia kubaini ukweli na kuwezesha Serikali kuchukua hatua zinazostahili kwa mujibu wa sheria.

Mkutano huo ulihudhuriwa pia na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Ndugu Chiza Marando

Serikali imesisitiza kuwa uchunguzi utafanyika kwa haki, uwazi na kwa kuzingatia sheria ili kulinda maslahi ya wananchi na kuimarisha utawala bora.



ZAIDI YA ULINZI NA USALAMA: POLISI RUVUMA WAONESHA UPANDE MWINGINE WA HURUMA HOSPITALI YA HOMSO

Wakati wengi huliona Jeshi la Polisi likitekeleza majukumu ya ulinzi na usalama, Julai 30, 2026 limeandika sura nyingine ya huduma kwa jamii baada ya kuwafariji wazazi waliojifungua katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea (HOMSO) kwa kuwapatia mahitaji muhimu kwao na watoto wachanga.

Msaada huo ulitolewa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Ruvuma kupitia Kitengo cha Usalama Barabarani, kwa kushirikiana na Kitengo cha Polisi Jamii, ikiwa ni sehemu ya kuimarisha uhusiano kati ya polisi na wananchi kupitia matendo ya huruma.

Bidhaa zilizokabidhiwa zilijumuisha mahitaji muhimu ya akina mama na watoto wachanga, yakilenga kupunguza changamoto zinazowakabili familia katika siku za mwanzo baada ya kujifungua.

Hatua hiyo inaendeleza falsafa ya polisi kushiriki moja kwa moja katika shughuli za kijamii zinazogusa maisha ya wananchi, sambamba na jukumu lao la msingi la kulinda amani na usalama.







FARAJA KWA WAKAZI WA KILAGANO! DKT. BUNUNGU AKABIDHI AMBULANCE, HUDUMA ZA DHARURA KUBORESHWA ZAIDI

Safari ndefu za kutafuta huduma za dharura sasa zinatarajiwa kupungua kwa wananchi wa Kata ya Kilagano Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma baada ya Mbunge wa Jimbo la Peramiho, Dkt. Lazaro Komba (Bunungu), kukabidhi rasmi gari la kubebea wagonjwa (ambulance) katika Kituo cha Afya Kilagano .

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Dkt. Bunungu, alisema ambulance hiyo itarahisisha usafirishaji wa wagonjwa wanaohitaji rufaa kwenda kwenye hospitali za ngazi ya juu, hivyo kuongeza kasi ya huduma za dharura na kuokoa maisha.

Alisisitiza kuwa gari hilo libaki muda wote katika Kituo cha Afya Kilagano na litumike kwa malengo yaliyokusudiwa ili wananchi wapate huduma kwa wakati bila vikwazo.

Ambulance hii ni tumaini jipya la kuokoa maisha na kuimarisha huduma za afya kwa maelfu ya wananchi.



USIPITE BILA KUTEMBELEA! TEKNOLOJIA ZA KISASA ZINAZOVUTIA MBINGA

Kama unadhani kilimo bado ni cha jembe la mkono, basi maonesho yanayoendelea katika viwanja vya Amani Makoro wilayani Mbinga Mkoani Ruvuma yatakubadilisha kabisa mtazamo.

Teknolojia za kisasa, mbegu bora na mashine za kuongeza thamani ya mazao ndivyo vinavyowavutia mamia ya wageni.

Akitembelea maonesho hayo, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Andrew Mbunda, alikagua mabanda ya kilimo na ujasiriamali, vipando vya mazao mbalimbali pamoja na mashine za kisasa zinazosaidia kuongeza uzalishaji na thamani ya mazao.

Mbunda aliwapongeza wataalamu wa kilimo kwa maandalizi yaliyofanikisha maonesho, huku akitoa mwaliko kwa wananchi kutembelea banda la Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kupata elimu kuhusu kilimo-biashara, matumizi sahihi ya viatilifu, mbegu bora na teknolojia zinazoongeza tija na kipato.

Wakati huo huo Maonesho ya Nanenane ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yanaendelea jijini Mbeya yanawakutanisha washiriki kutoka mikoa saba Mbeya (mwenyeji), Ruvuma, Iringa, Njombe, Songwe, Katavi na Rukwa yakitoa fursa ya kujifunza, kuwekeza na kuimarisha sekta ya kilimo.



BRIGEDIA JENERALI AHMED ABBAS AHMED ASHIRIKI UFUNGUZI WA NANE NANE NYANDA ZA JUU KUSINI MBEYA

Maonesho ya Nane Nane kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yameanza rasmi katika Viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya, yakikusanya maelfu ya wananchi, wakulima, wafugaji, wavuvi na wadau wa maendeleo kwa lengo la kuonesha ubunifu unaochochea mapinduzi ya sekta ya kilimo.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, ameshiriki katika hafla ya ufunguzi wa maonesho hayo, yaliyowakutanisha viongozi wa Serikali, taasisi mbalimbali na wadau wa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kutoka mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Maonesho hayo yanatoa jukwaa la kubadilishana maarifa, kuonesha teknolojia za kisasa za uzalishaji, kuhamasisha matumizi ya mbegu bora, pembejeo na mifumo ya kisasa ya kilimo yenye tija, huku yakifungua fursa za uwekezaji, biashara na ushirikiano kati ya wazalishaji na sekta binafsi.

Ushiriki wa viongozi wa Serikali unadhihirisha dhamira ya kuendelea kuimarisha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kama nguzo muhimu ya uchumi na maendeleo ya wananchi.



JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA
Kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

S.L.P 74 SONGEA
57180 RUVUMA
SIMU Nambari; 025-22602256/2602238
FAX Na.2602144
E-EMAIL: ras.ruvuma@tamisemi.go.tz
TOVUTI: www.ruvuma.go.tz
INSTAGRAM: rs Ruvuma
FACEBOOK: rs Ruvuma
YOUTUBE: rs ruvuma